



Karibu Maktabani

*“Mtu anaweza kuelewa kwa maneno.
Mtu anaweza kujieleza kwa maneno.
Na maneno yanatusaidia kuishi na wengine”.*

BENKT-ERIK HEDIN

Mtoto anayepata kusikia hadithi na masimulizi mapema katika maisha yake, hujipatia lugha tajiri. Kumsomea mtoto kwa sauti ni njia bora ya kuendeleza lugha na mawazo ya mtoto.

Unaweza kumsaidia mtoto wako apate lugha tajiri kwa kumsikiliza na kuzungumza naye. Yote unayofanya pamoja na mtoto wako yanamsaidia apate lugha bora. Usume, uimbe, umhadithie. mweleze, ucheze naye mtoto wako! Fanya hivyo mapema utotoni, tangu mwanzoni, kwani wakati wa mwanzoni ndipo msingi wa lugha unawekwa.

Ogea na mtoto wako kwa lugha yako mwenyewe. Kama mtoto akipata lugha tajiri ya kwanza (lugha ya mama/mzazi), basi ataweza kujifunza lugha ya pili kwa urahisi zaidi.

Katika maktaba vipo vitabu vya watoto wa kila umri. Vipo vitabu vya kusoza kidole kwa watoto wadogo kabisa, vitabu vya picha, vitabu vyenye vina na nyimbo za watoto, vitabu vya mashairi, vitabu vya hakika, vitabu vya hadithi na masimulizi.

Katika maktaba vipo vitabu kwa watu wa kila umri na kwa lugha nyingi. Tungependa kukusaidia kuvitafuta vitabu unavyovitaka. Na kuazima vitabu ni bila malipo yoyote!

Maktaba ina vilevile vitabu kwa watu wazima kuhusu magonjwa ya watoto, saikolojia ya watoto (elimu-nafsi), malezi ya watoto, na kadhalika. Maktaba ina vitabu kwa lugha nyingi, kwa watoto na watu wazima pia.

Karibu!

